

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini

**HOTUBA YA MKUU WA WILAYA YA UBUNGO KATIKA UFUNGUZI
WA MAFUNZO YA KUKATA TIKETI KWA NJIA YA MTANDAO**

Tarehe: 7 Mei 2020

Mahala: KITUO CHA KIMATAIFA CHA MABASI MBEZI LUIS

Ndg. Katibu Mtendaji Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini,

Mkuu wa Polisi Kituo cha Mabasi Mbezi Luis;

Viongozi Mbalimbali,

Washiriki wa mafunzo,

Waandishi wa Habari Mabibi na Mabwana

Habarini za Asubuhi.

Awali ya yote natoa shukrani za kipekee kwa kunialika katika shughuli hii muhimu ya Ufunguzi Mafunzo ya kukata tiketi kwa njia ya Mtandao.

Nawashukuru wadau wote kwa kukubali kuhudhuria mafunzo haya muhimu katika kusaidia Sekta ya Usafiri Nchini kwenda mbele. Ninatambua kila mmoja wetu ana majukumu mazito ya kiofisi au binafsi lakini kwa kutambua umuhimu wa mafunzo haya ameacha shughuli zake ili kwa pamoja tuweze kushirikiana.

Ndugu wa Shiriki,

Watanzania walio wengi wanatumia usafiri wa barabara katika shughuli zao za kila siku za kijamii na kiuchumi. Usafiri wa barabara hapa Tanzania na katika nchi nyingine zinazoendelea unakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo matumizi duni ya teknolojia kurahisisha huduma za usafiri.

Ndugu Washiriki,

Tafiti nyingi zinaonyesha kuwa, nchi nyingi zilizopiga maendeleo katika Uchumi, ni zile zinazotumia mfumo madhubuti ya kiteknologia na kuwa na kumbumbu sahihi kwa ajili ya mipango endelevu ya mataifa hayo. Nasi Tanzania haunabudi kuhamasishana na kuwa na Azma Moja ya kutumia teknolojia iliyopo hivi sasa ya ukataji tiketi kwa njia ya Mtandao.

Nimeambiwa kuwa, Mfumo wa Tiketi Mtandao umetengenezwa kwa kuzingatia mahitaji mbalimbali ya kiwemo ya Abiria, Wamiliki wa Mabsi na Serikali:

- i. Kurahisisha maisha ya abaria wetu katika ukataji wa tiketi na kufanya malipo bila kulanguliwa hususan vipindi vya sikukuu za mwisho wa mwaka
- ii. Kuzingatia na kurahisisha mahitaji ya abiria wasio na simu janja
- iii. Mfumo utatatua changamoto nyingi katika Sekta yetu ya Usaafiri wa Abiria

Ndg Washiriki,

Mfumo wa ukataji tiketi kwa njia ya Mtandao, unafaida kwa makundi mbalimbali, na kwa abiria faida hizo ni pamoja na

Kwa abiria

- Kuokoa muda na gharama za kwenda kukata tiketi kwenye vituo vya mabasi.
- Kuepuka usumbufu wa kukata tiketi katika vituo vya mabasi.
- Kuepuka adha ya upandishwaji wa nauli holela /ulanguzi
- Kupata basi ambalo ni chaguo lake
- Kuwa na uhakika wa kupata nafasi (siti) kwenye basi siku ya safari.
- Atakuwa na kumbukumbu ya kudumu kuhusu safari yake

Kwa wamiliki wa mabasi

- Kupata fedha zao kiurahisi
- Kuondokana uvujaji wa makusanyo
- kuwa na kumbukumbu ya kudumu kwa abiria wote wanaosafiri.
- Kupunguza gharama za uendeshaji.

- Kukopesheka kwa urahisi kutokana na taarifa za fedha kuwa bayana
- Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa biashara yake
- Kuwa na taarifa ya idadi ya abiria kwenye mabasi yake muda wowote

(c) Kwa serikali

- Kupata takwimu sahihi na za kutosha zinazohusiana na sekta za usafirishaji.
- Kuiwezesha serikali kutambua maeneo yenye kipaumbele cha Ujenzi wa Miundombinu na uwekezaji wa huduma za usafiri.

Ndg Washiriki,

Kama mnavyofahamu, Kituo Cha JPM cha hapa Mbezi Luis, ni kituo Cha Kimataifa na ni cha Kwanza kwa Ukubwa, na chenye uwezo wa kuhudumia mabasi yaendayo Nchi Mbalimba Katika Afrika Mashariki na Nchi wanachama wa SADC. Ili kituo hiki kiendeleo kuwa cha Mfano, tunahimiza matumizi sahihi ya kieletroniki katika ukatishaji tiketi kwa abiria na Mizigo yao.

Nitoe Wito kwa abiria Wote wanaotumia kituo hiki, Kama ilivyo kwa Biashara nyingine Tanzania, Ukinunua kitu dai risiti ya EFD, na kwa abiria, ukilipa nauli dai tiketi ya Kielektroniki au kata mwenyenye kielektroniki.

Kwa Wamiliki wa Mabasi, tumieni teknolojia zilizopo kutoa tiketi za kielektroniki.

Baada ya kusema hayo, natamka kuwa, Mafunzo yenu yamefunguliwa Rasmi.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo.